Nairobi Journal of Humanities and Social Sciences

NJHS



https://doi.org/10.58256/crqt7f28

Research Article

Section: Literature, Linguistics & Criticism

Check for updates

Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global.

Volume 8, Issue 1, 2024

**Article Information**
Submitted: 11th January 2024
Accepted: 18th March 2024
Published: 14th April 2024

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

ISSN: 2520-4009 (Print)
ISSN: 2523-0948 (Online)

To read the paper online, please scan this QR code

**How to Cite:**
Musyoki, P. M., Makoti, V., & Mutua, J. (2024). Ubainishaji wa Vigezo vya Utoaji wa Toponemia Katika Jamii ya Wakamba: Mfano Kutoka Jimbo dogo la Makueni, Kenya. *Nairobi Journal of Humanities and Social Sciences, 8*(1). https://doi.org/10.58256/crqt7f28

# Criteria for analysing Kamba toponyms: A case study of Makueni Sub-County, Kenya

**Peninah Mwende Musyoki, Vifu Makoti, John Mutua**
Department of Linguistics and Languages, Machakos University, Kenya
Corresponding Email: peninahmwendem@gmail.com

**Abstract**
This article investigates the criteria for giving of toponyms in the Kamba community with reference to an example from Makueni Sub County in Kenya. The data used herein was part of the larger data collected from all the eleven (11) locations of Makueni sub county. Data was obtained from twenty-two (22) men all aged sixty (60) years and above. The sample of respondents was selected randomly. The men were easily obtained because their details were kept in the chiefs' offices for the record of the social welfare program from the national government. The study found that toponyms in the selected area were issued after considering certain criteria like physical appearance of a place, community activities, and historical events amongst others. This paper provides relevant and usefull references for future researchers who may look into different aspects of Onomastics in the Kamba community and other communities.

**Keywords:** criteria, lexical aanlysis, onamastics, toponyms

© 2024 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

https://doi.org/10.58256/crqt7f28

Research Article

Section: Literature, Linguistics & Criticism

Check for updates

Published in Nairobi, Kenya by Royallite Global.

Volume 8, Issue 1, 2024

**Article Information**
Submitted: 11th January 2024
Accepted: 18th March 2024
Published: 14th April 2024

Additional information is available at the end of the article

https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/

ISSN: 2520-4009 (Print)
ISSN: 2523-0948 (Online)

To read the paper online, please scan this QR code

# Ubainishaji wa Vigezo vya Utoaji wa Toponemia Katika Jamii ya Wakamba: Mfano Kutoka Jimbo dogo la Makueni, Kenya

**Ikisiri**

Makala hii inachanguza vigezo vya utoaji wa toponemia katika jamii ya Wakamba kwa kurejelea mfano kutoka Jimbo dogo la Makueni nchini Kenya. Data iliyotumika ilikusanywa kutoka kata zote kumi na moja (11) za jimbo dogo la Makueni. Data hiyo ilipatikana kutoka kwa wasailiwa ishirini na wawili (22) waliokuwa na umri wa miaka sitini (60) na zaidi. Wazee hao walichaguliwa kwa usampuli nasibu. Sampuli hii ya wazee ilipatikana kwa urahisi kwa kuwa majina ya wazee hao yamehifadhiwa katika ofisi za machifu kwa sababu ya rekodi za marupurupu ya uzeeni wanayopokea kutoka kwa serikali kuu. Uchunguzi huu ulibaini kuwa toponemia katika eneo teule zilitolewa kwa kuzingatia vigezo kama vile sifa za kimaumbile, shughuli za kijamii, matukio ya kihistoria na vingine. Kazi hii itatoa marejeleo muhimu kwa watafiti wa baadaye watakaoshughulikia vipengele tofauti vya Onomastiki katika jamii ya Wakamba na jamii nyingine.

**Istilahi muhimu:** Jamii, Toponemia, Ubainifu, Utoaji, Vigezo

**How to Cite:**
Musyoki, P. M., Makoti, V., & Mutua, J. (2024). Ubainishaji wa Vigezo vya Utoaji wa Toponemia Katika Jamii ya Wakamba: Mfano Kutoka Jimbo dogo la Makueni, Kenya. *Nairobi Journal of Humanities and Social Sciences, 8*(1). https://doi.org/10.58256/crqt7f28

© 2024 The Author(s). This open access article is distributed under a Creative Commons Attribution (CC-BY-NC-SA) license.

## UTANGULIZI

Onomastiki ni Sayansi inayochunguza majina kwa jumla. Taaluma ya Onomastiki imegawika katika sehemu mbili kuu; Anthroponemia (majina ya binadamu) na Toponemia (majina ya mahali). Toponemia ni tawi la Onomastiki linaloshughulikia majina ya mahali. Sehemu mbalimbali hupata majina kutokana na uasili wake (Crystal, 1987). Rye (2006) na Raybum (2010) wameshughulikia taaluma ya Onomastiki kwa kutumia mkabala wa kiisimujamii. Wataalamu hao walibainisha mambo mbalimbali ya kiisimu yanayosababisha uteuzi wa toponemia. Rugemalira, (2009) na Buberwa, (2011) walionyesha uamilifu wa viambishi ngeli katika majina ya mahali. Mjapelo, (2009) alizingatia mkabala wa kimofolojia kushughulika taaluma ya Onomastiki. Kihore na wenzake, (2004) na Mwanamseke, (2011) walitafiti kuhusu vipengele vya kimofolojia vya nomino za Kibantu kwa kujikita katika nomiono za kawaida. Walidai kuwa nomino mahususi huundwa kwa mzizi tu na haziwezi kuchanganuliwa kimofolojia. Madai haya yaliungwa mkono na Habwe, (2007) aliyeshikilia kwamba nomino za pekee kama vile za mahali hujidhihirisha katika maumbo yake maalumu. Makali hii inaangalia nomino kama toponemia na sifa zinazoshabihiana na toponemia hizo. Kwa mfano, jina *Kithoni* katika lugha ya Kikamba ni mahali palipo na chemichemi ya maji.

Kahigi, (2007) alishughulikia mbinu ya eponimu ambayo inahusu utoaji wa majina ya mahali kutokana na majina ya watu. Masamba, (2004) alishugulikia mbinu ya uhamishaji maana inayohusisha maneno ambayo tayari yanatumika katika lugha fulani na kuyapa maana nyingine mpya. Micheni na wenzake, (2022) walichunguza vigezo vya utoaji wa majina katika jamii ya Maara nchini Kenya. Kuna watafiti wengine waliochunguza majina kwa jumla. Kwa mfano, Musyimi, (2011) alichunguza maana, ishara maana na misingi ya kitamaduni ya majina ya watu katika jamii ya Wakamba nchini Kenya. Makoti, (2006) alichunguza majina ya watu katika jamii ya Wadigo nchini Kenya. Kirui, (2013) alifanya uchunguzi wa kimofosemantiki wa majina ya mahali katika jamii ya Kipsigis nchini Kenya. Karama (2022), alichunguza toponemia za mitaa ya mji wa Mombasa.

Japo kipengele cha majina kinaoneka kushughulikiwa na wanaisimu mbalimbali. Tafiti hizi ziliegemea zaidi katika semantiki ya majina ya watu na ya mahali. Kazi hii ilishughulikia kwa kina vigezo vya utoaji wa toponemia katika jamii ya Wakamba.

## JAMII YA WAKAMBA

Wakamba ni wa kundi la watu liitwalo Wabantu ambao huishi katika sehemu ya mashariki ya nchi ya Kenya hasa katika Majimbo ya Machakos, Kitui na Makueni. Eneo hilo wanaloishi huoitwa Ukambani (Mathooko, 2004). Wakamba ndio kabila la pili kwa idadi katika majimbo manane yakiwemo Mombasa na Nairobi. Wanaoongea lugha ya Kikamba. Lugha yao ina uhusiano wa karibu na lugha zingine za Kibantu kama za Kikuyu, Kiembu, Kimbeere na Kimeru. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2019, Wakamba wote walikuwa 4,663,910 kwa idadi.

Kama jamii nyingine ulimwenguni, Wakamba wana majina yanayotaja watu mahali na vitu mbali mbali katika mazingira yao. Walikuwa na utaratibu maalum wa kupata majina ya watu. Mtoto wa kwanza wa kiume alipewa jina la babu yake upande wa baba na wa pili upande wa mama yake. Akiwa wa kike aliitwa jina la nyanya yake upande wa baba na wa pili upande wa mama yake. Watoto aliofuata walipewa majina ya kurejelea vigezo fotauti kama vile; majira aliyozaliwa mtoto, hali ya anga iliyotawala wakati wa kuzaliwa kwa mtoto na vingine. Hii inadhihirisha kuwa jamii ya Wakamba ilichukulia shughuli ya utoaji wa majina kwa uzito na kwamba kulikuwa na mfumo maalum waliofuata.

### Vigezo Vilivyozingatiwa Katika Utoaji wa Majina Katika Jamii ya Wakamba

Makala hii imebainisha vigezo kadhaa vilivyozingatiwa katika utoaji wa toponemia katika jamii ya Wakamba. Vigezo hivyo ni pamoja na kuwepo kwa miti na mimea, kuwepo kwa wanyama na ndege mahali fulani, shughuli za kijamii, sifa za kimaumbile za mahali na majina ya watu maarufu waliowahi kuishi mahali fulani. Ufuatao ni ufafanuzi wa vigezo vilivyotumiwa kupata majina ya mahali katika eneo la jamii

ya Wakamba.

**Shughuli za Kijamii**

Kulingana na data iliyopatikana, jamii ya Wakamba ilipata baadhi ya majina ya mahali kwa kuzingatia shughuli zilizoendelezwa na wanajamii katika sehemu husika. Shughuli hizo zilikuwa za kiuchumi au za kitamaduni. Toponemia zifuatazo zinathibitisha maelezo haya.

*Ngiitini* ni jina linalotaja Kijiji kimojawapo katika kata ya Kivani. Linataja aina ya miti iliyotumiwa katika ujenzi wa nyumba za kienyeji. Sehemu iliyo na jina hilo ilikuwa na wingi wa miti iliyotumika kwa shughuli hiyo. Watu kutoka sehemu mbalimbali walifika hapo ili kuitafuta. Nyumba zilizohitaji aina hii ya miti zimepungua na kupoteza umaarufu wake. Hali hii imechangiwa na maendeleo ya kiuchumi na kiteknolojia ambayo yamewafanya Wakamba waanze kujenga nyumba za kisasa. Japo shughuli iliyosababisha jina hiyo ilipitwa na wakati na kuachwa na wengi, jina la mahali hapo limebaki vilevile.

*Ndivuni* ni toponemia inayotumika kurejelea kijiji kimojawapo katika kata ya Kivani. Jina hili linarejelea josho. Lina maana ya mahali pa 'kuoshea' mifugo ili kuua wadudu wategemezi kama vile kupe na chawa. Jina hili limeundwa kwa nomino *Ndivu* na kielezi *-ni* cha mahali. Wakamba walipata neno hilo wakijaribu kutamka *dip* ambalo ni neno la Kiingereza. Palikuwa na mjengo uliokuwa na Kidimbwi chenye kina kilichowezesha kufunikwa kwa wanyama hata mafahali wenye kimo kikubwa. Upande wa pili wa Kidimbwi hilo kulikuwa na vidaraja ambavyo wanyama walitumia kujitoa mle ndani baada ya kutumbukizwa kwenye maji yaliyochanganywa na dawa. Katika sehemu ya kuingilia kulikuwa na njia nyembamba iliyojengwa kwa miti na ilisaidia kuwapanga hao wanyama katika foleni ili waingie pale mmoja mmoja. Jina la mahali hapa lililingana vizuri na shughuli iliyoendelezwa na wanajamii katika sehemu husika. Karibu kila sehemu iliyo na josho katika maeneo ya Ukambani huitwa *Ndivuni*.

*Kee* ni jina linalorejelea kata na pia kata ndogo. Linatokana na kitenzi *kukeewa* kinachomaanisha "kuchewa." Jina hili lilitokana na shughuli ya wizi wa mifugo. Wakamba walipotoka kuiba mifugo kutoka kwa Wamaasai walikuja kutulia hapo hadi wakati wa mapambazuko. Walipenda mahali hapo kwa sababu palikuwa tambarare kiasi pakilinganishwa na kwingine walikopitia kwenye milima. Jina hili linatumika kurejelea mahali hapo hata baada ya shughuli iliyolisababisha jina lenyewe kuisha.

*Kyamwalye* ni jina la kijiji katika kata ya *Kee* linalotokana na kitenzi *Kwalya* chenye maana ya "kuchanja." Mwanzoni paliitwa *Muteta* kwa sababu palikuwa na miti mingi ya *Miteta*. Miti hiyo ilikuwa mizuri kwa kuni kwa hivyo watu kutoka sehemu zingine wangefika pale wakiwa na mashoka ili kuchanja kuni. Idadi ya watu ilipozidi kuongezeka, shughuli hiyo ya kuchanja kuni ilizidi hata ikasababisha kupungua kwa miti hiyo. Shughuli hii ya kuchanja kuni ilipata umaarufu kutokana na wingi wa watu waliohusika. Hali hii ndiyo ilisababisha kubadilika kwa jina la mahali hapa pakaanza kuitwa *Kyamwalye* badala ya *Muteta*.

*King'ang'a* ni jina la kijiji katika kata ya Kee. Linatokana na kitenzi *kung'ang'a* kilicho na maana ya "kushika au kufunga kitu kwa nguvu za mtu zote." Jina hili lilitokana na shughuli ya kupimana nguvu iliyofanywa na vijana kwa madhumuni ya kuwaburudisha waliotazama. Vijana barobaro walioitwa *nthele* katika lugha ya Kikamba wangekutana mahali maalumu ili kushindana nguvu huku mashabiki wakiwashangilia. Huko kushindana nguvu ndiko *kung'ang'ana*. Hii inadhihirisha kwamba shughuli hii ilikuwa maarufu miongoni mwa Wakamba.

**Majina ya Miti na Mimea Tofauti**

Ilibainika kuwa utoaji wa toponemia katika eneo husika ulizingatia kigezo cha kuwepo kwa miti na mimea tofauti katika sehemu fulani. Kulingana na wenyeji sio miti yote iliyotumika kutambulisha mahali bali ile ilikuwa na manufaa fulani kwa jamii kama vile kutumika katika ujenzi, matunda yake yaliliwa, watu walibarizi chini yake, n.k. Toponemia zifuatazo zilitokana na aina ya miti au mimea iliyopatikana mahali fulani.

*Ndumani* ni jina linalorejelea kijiji fulani katika kata ya Watema. Linatokana na nomino *nduma*

kwa maana ya "viazi vikuu," na kiambishi "ni" kinachotumika kuashiria "mahali katika lugha ya Kikamba. Kwa mujibu wa wakazi waliosahiliwa, sehemu hii ambayo iko chini ya milima ya *Kilungu* ilikuwa na maji yaliyotiririka kutoka milima hiyo. Kuwepo kwa maji kuliwezesha upanzi wa viazi vikuu kwa wingi ndipo watu wakapaita *Ndumani* (mahali pa viazi vikuu). Jina hili lina mlingano na shughuli iliyosababisha sifa iliyozua jina lenyewe. Wafanya biashara kutoka sehemu mbalimbali hasa kina mama walifika hapo ili kupata bidhaa hii. Kwa mujibu wa wenyeji sehemu hii bado inakuzwa viazi vikuu lakini si kwa wingi kama ilivyokuwa hapo zamani kwa sababu maji yamepungua kwa kiasi kikubwa kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

*Muvau* ni jina la mojawapo ya kata katika Jimbo dogo la Makueni. Limetokana na aina ya mti (*muvau*) uliopindwa bila kukatika na hivyo ukawa unatumiwa katika kutengenezea upinde. Miti hiyo ilijulikana sana kwa sababu pinde na mishale ndizo zilikuwa silaha kuu za vita miongoni mwa Wakamba. Walitumia silaha hizi kuwakabili maadui wao na wanyama hatari waliowatishia maisha. Silaha hizi zilitumiwa pia katika shughuli za uwindaji. Wawindaji hodari waliwarithisha watoto wa kwanza wa kiume pinde maalum kama ishara ya kuwaachia kipawa hicho cha uwindaji. Wenyeji waliongeza kuwa pinde zilikuwa mojawapo ya vifaa vya wanganga japo hawakuwa na uhakika wa matumizi yake katika shughuli hizo za unganga. Maelezo hayo yanaonyesha kuwa pinde zilikuwa vifaa muhimu miongoni mwa jamii ya Wakamba. Kwa mujibu wa wakazi waliosahiliwa, watu wangetoka sehemu za mbali kuja kufuata aina hii ya miti hapa kwa sababu haikuwa kila mahali. Hivyo, jina hili likaenea na kuwa maarufu miongoni mwa watu wa karibu na wa mbali.

*Katoloni* ni jina la kijiji katika kata ya Muvau. Linatokana na aina ya mti unaoitwa *kitoo* unaozaa matunda yanayoliwa. Matunda haya huwa na ladha tamu na huwa kama gundi mdomoni. Wakaazi wa eneo hili walieleza kuwa mti uliosababisha kuzuka kwa jina hili ulikuwa mdogo kuliko ilivyotarajiwa ikizingatiwa umri wake ndipo jina lake likawa katika hali ya udogo (*Katolo*) badala ya *kitoo* ambalo ndilo liko katika hali ya wastani. "ka" ni kiambishi kinachosimamia udogo katika lugha ya Kikamba. Wakamba walikuwa na kitendawili kilichotaja mti huu: *Nau muasa utandwiia itoo* (Baba mrefu lakini hawezi hunichumia tunda liitwalo *itoo*) - jibu ni *nzia* (Njia). Kitendawli hiki kinadhihirisha kuwa matunda haya yalipatikana kwa wingi ukambani na yalipendwa na watu wa jamii hii. Kwa mujibu wa wasahiliwa, miti hii haipo tena. Walikisia kwamba kumea na kukua kwa mti huu huwa kugumu ndiposa shughuli za watu na wanyama zilipoongeka miti hiyo iliisha katika eneo husika.

*Kiatine* ni jina la kata ndogo katika eneo linalotafitiwa. Jina hili linarejelea aina ya mti ambao mazao yake huitwa *miatine*. Mazao haya yalikuwa maarufu miongoni mwa Wakamba kwa sababu waliyatumiwa katika kutengenezea pombe ya kienyeji inayoitwa *kaluvu* kwa maana ya pombe ya kienyeji ya Wakamba. Watu wangetoka mbali kuja kutafuta hayo mazao kwa sababu miti hiyo haikuwa kila mahali. *Miatine* ilitumika kwa muda kisha inakuwa mizee na kupoteza huo uwezo wa kuchachuza pombe. Hii iliwalazimu watengenezaji wa pombe kurudi tena *Kiatine* kutafuta mingine. Hivyo mahali hapo palipata umaarufu kwa sababu ya kuwa na bidhaa iliyohitajika na watu wengi. Kwa mujibu wa wenyeji, mti huo haupo tena bali miti mingine ya aina tofauti ndiyo imemea pale.

**Sifa za kimaumbile za mahali**

Mandhari ya kijiografia ya mahali yalitumiwa kupata majina ya mahali. Sifa zilizotumiwa ni kama sehemu za kinamasi, maziwa, chemichemi za maji, vilima n.k. Ifuatayo ni mifano ya majina yaliyopatikana kwa kuzingatia sifa za mahali paliporejelewa.

*Yiani* ni toponemia inayotumika kutaja kijiji katika kata ya *Watema*. Inamaanisha "mahali pa kinamasi," katika sehemu hii maji mengi yalituama siku nyingi baada ya mvua kuacha kunyesha kwa kuwa hakukuwa na mteremko kwa hivyo maji hayakutiririka kwenda kwingineko. Pia mchanga wa sehemu hiyo ni ule usioruhusu maji kupita kwa urahisi. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi kinamasi hiki kimepungua kwa kiasi kikubwa na kubaki kuwa na maji tu wakati wa mvua. Japo sifa ya mahali hapa imezidi kudidimia,

jina hili halijabadilika. Kwa mujibu wa wenyeji waliosahiliwa, maji kutoka kwenye kinamasi hiki yaliwafaa kwa kuwanywesha mifugo na kwa shughuli za kinyumbani kama kufua nguo kwa sababu yalikuwa maenge. *Nthongoni* ni ni jina la kijiji na soko katika kata ya *Ukia*. Jina hili linalotokana na nomino *nthongo* ambayo inaamanisha "sehemu ambapo maji yanatoka ardhini; yaani chemichemi ya maji". Ni kisawe cha *kitho*. Kiambishi tamati "ni" kinaashiria mahali katika lugha ya Kikamba. Sehemu iliyopewa jina hili ina maji ya aina hii. Jina hili limetumika kijazanda kwa sababu maana asilia ya neno *nthongo* ni chongo. Jicho lenye chongo huwa halinyauki kabisa; kila wakati huonekana yakiwa na unyevunyevu. Sifa hii ndiyo ilitumiwa ili kufananisha hali hizi mbili. Kwa mujibu wa wenyeji, maji yaliyotoka katika chemichemi hiyo yalikusanyika na kuwa kidimbwi. Maji yalipojaa katika kidimbwi hicho yalitiririka upande wa chini na kuwa kijito. Tofauti na ilivyokuwa hapo zamani, siku hizi hakuna kijito kinachotiririka kutoka kidimbwini isipokuwa wakati wa mvua lakini chemichemi yenyewe bado iko.

*Manyanzala* ni jina la kijiji. Linatokana na wingi wa nomino *inyanzala* ambayo iko katika hali ya ukubwa. Jina hili lina maana ya mawe makubwa yaliyoenea sehemu kubwa lakini yasiyoinuka juu. Kiambishi awali "-ma" kinaashiria wingi wa nomino iliyo katika kundi la YA-MA. Mawe haya yanapatikana kwa wingi ndani ya mto unaoitwa *Thiva* ulio katika kata ya *Ukia*. Kwa mujibu wa wenyeji, mawe hayo yaliibuliwa na mmomonyoko wa udongo katika sakafu ya mto huo.

**Majina ya ndege na wanyama**

Utafiti umedhihirisha kuwa kuna baadhi ya majia ya mahali katika eneo la utafiti ambayo yalitokana na kuwepo kwa Wanyama na ndege walioishi mahali husika. Viumbe hao walikuwa na sifa mahususi kama vile kula kuku, kuwa wengi mahali fulani au walikuwa na sifa za kimaumbile zilizowastaajabisha watu.

*Kya Nzivu* ni jina la kijiji katika kata ya *Ikuua*. Lilitokana na jna la wanyama wadogo wa familia ya paka ambao huwa wasumbufu sana kwa kula kuku. Wanyama hao wanaitwa *nzivu* kwa maana ya monzo "paka mwitu". Walikuwa wengi katika msitu uliokuwa katika mlima. Katika lugha ya Kikamba, mlima huitwa *kiima*. Kwa hivyo, *Kya Nzivu* ni toponemia iliyoundwa kwa kiwakilishi cha a– unganifu (*Kya*) kurejelea mlima na jina la wanyama hao (*Nzivu)*. Sifa ya usumbufu ya wanyama hawa ilieleweka na wakazi wote wa eneo hilo kwa sababu walikuwa kero kwa wote waliofuga kuku. Kwa hivi sasa wanyama hawa wamehamia sehemu za juu za mlima huo na wengine kuhamia sehemu zingine zilizo na vichaka vinavyotosha kuwasetiri na utulivu wanaohitaji. Kutokana na wingi wa wanyama hawa na tabia yao mahali hapa paliitwa jina lao "*Nzivu*" na "*Kya*" ambacho ni kiwakikishi cha *kiima* (mlima). Kwa hivyo maana ya jina hili ni mlima uliokuwa na *Nzivu* (monzo) wengi.

*Nthimbani* ni jina la kata ndogo. Eneo hilo lilijulikana na wengi kwa sababu lilikuwa madhabahu ambapo wazee walienda kwa kusudi la kuabudu na kutoa kafara. Jina lenyewe lilitokana na aina fulani ya wanyama mwitu waitwao *nthimba* kwa maana ya "fungo". Kiambishi "-ni" kinaashiria mahali. Kwa hivyo jina hilo lilimaanisha mahali penye *nthimba* (fungo). Wanyama hawa wana tabia ya kunya mahali pamoja kwa muda mrefu. Kila mmoja hutengeneza mrundiko wake mkubwa wa kinyesi. Kilichowastaajabisha wenyeji kuhusu mnyama huyu ni kwamba hawakuona alama za miguu alikokanyaga akikunya katika kilele cha mrundiko ule. Hii iliwafanya watu wengine kufikiria kuwa mnyama huyo huwa na mbawa ambazo humsaidia kunya akipaa. Kuwepo kwa wanyama hawa katika eneo hilo ndiko kulisababisha jina la mahali hapo. Kwa hivyo jina hili linaonyesha mlingano wa wazi na kinachorejelewa.

*Ndue nguu* ni toponemia ambayo imeundwa kwa nomino na kivumishi chake. Inarejelea kijiji katika kata ya *Muvau*. Nomino *ndue* ni aina ya nyani anayeitwa "mbega" na *nguu* ni kivumishi kinachotokana na nomino *ukuu* kwa maana ya "uzee." Kwa hivyo jina hili lina maana ya mbega aliyekuwa mzee. Kwa mujibu wa wenyeji wa eneo hili, nyani hawa waliishi katika mlima ulio na jina hili lakini wakaondoka kufuatia ongezeko la watu na mabadiliko ya tabianchi. Walipokwisha kuondoka, mmoja wao alilemewa na uzee na wenzake wakamwacha pale. Mbega huyo mzee alibaki kwenye ule mlima pekee yake akisononeka kwa upweke ndiposa mahali hapo pakaitwa jina hili. Vizazi vya sasa huwa vinaadithiwa kuhusu wanyama

hao kwa kuwa hawako tena. Mmoja wa wasahiliwa alieleza kuwa wanyama hao walihamia sehemu za Mlima Kenya.

**Majina Yaliyotokana na Watu Maarufu**

*Kwa Kombo* ni jina linalotaja kijiji katika kata ya *Kee*. Lilitokana na jina la mtu aliyeitwa Kombo. Mtu huyu alikuwa maarufu kwa sababu alikuwa mfanyi biashara mtajika kijijini. Kombo alikuwa akiuza maziwa katika kijiji hicho. Kutokana na umaarufu wa mwanabiashara huyo, watu walianza kuita sehemu hiyo kwa jina lake. Maziwa yalihitajika kila asubuhi katika kila familia kwa sababu ndiyo yalitumika katika kutayarisha staftahi na vyakula vya watoto wadogo. Kwa hivyo, watu wengi ambao hawakuwa na ng'ombe walilazimika kufika kwa Kombo ili kupata bidhaa hiyo. Mwanabiashara huyo aliaga dunia kitambo lakini watu wa ukoo wake wako japo hawajajenga palipokuwa makao ya babu yao. Kijiji hicho bado kinaitwa "Kwa Kombo" ingawa ilidhihirika kwamba kuna kizazi ambacho hakina habari kuhusu asili ya jina hilo.

*Kwa Vilivu* ni jina la Kijiji kilicho katika eneo ya Mumbuni. Toponemia hii inatokana na jina la mtu aliyeitwa Phillip lakini Wakamba wakalitamka kwa *Vilivu*. Mahali hapa paliitwa jina la mtu huyo kwa sababu alikuwa maarufu katika kilimo. Alikuwa hodari katika ukuzaji wa mahindi na matunda kama machungwa machenza. Mkulima huyo alijulikana na kuwa wa kupigiwa mfano katika eneo zima ya Mashariki mwa chini ya nchi ya Kenya. Watu walisafiri kutoka mbali kwenda kujionea kilimo. Wasahiliwa walisema kuwa *Vilivu* alipanda mahindi moja moja huku akiacha nafasi iliyopendekezwa katikati ya mimea hiyo. Pia alitia mbolea iliyotokana na mifugo katika mashamba yake na hivyo kuboresha mazao. Umaarufu wake ulimfikia aliyekuwa Rais wa pili wa Jamuhuri ya Kenya; Hayati Mzee Daniel Arap Moi aliyempa tuzo mbalimbali.

**Upatikanaji wa Vitu Maalum**

Kwa mujibu wa data iliyopatikana kutokana na mahojiano ya ana kwa ana na wazee, baadhi ya toponemia zilitokana vitu maalum vilivyopatikana katika katika maeneo fulani. Mifano ya vitu hivyo ni kama mawe, mito, mabonde na vitu vingine vilivyotengenezwa na binadamu.

*Mutheeti* ni toponemia inayotaja kijiji kilicho katika kata ya *Nziu*. Inatokana na kitenzi *Kutheeta* ambacho kina maana ya kutenganisha nafaka kama mtama na maganda yake baada ya kuzitwangwa. *Mutheeti* ni mtu anayetekeleza kitendo hicho. Jina hili linarejelea kijiji kingine katika kata ya *Nziu*. Kulingana na wenyeji waliosahiliwa, sehemu hii ilikuwa ikilimwa mtama kwa wingi. Wakati wa kuvuna watu wangepeleka mtama wao mahali maalumu palipokuwa na jiwe lililokuwa tambarare juu na lililoenea mahali pakubwa. Wakulima hawa walifanya hivi kwa zamu. Kwa hivyo mahali penyewe pakawa na umuhimu kwa wenyeji ndipo wakapapaita jina lililorejea shughuli iliyotekelezewa hapo. Jiwe hili bado liko japo sasa ni milki ya mtu binafsi bali si ya jamii pana kama ilivyokuwa zamani.

*Itangini (kwa Nomani*) ni jina la Kijiji na mji mdogo ambao una umaarufu wa kuwa soko kuu la matunda tofauti. Jina hili lilitokana na ujenzi wa tangi kubwa la maji lililojengwa na mzungu ili wenyeji na wanyama waweze kupata maji safi ya kunywa. Kwa mujibu wa wenyeji, Mzungu huyu alipokamilisha mradi huo alitangaza kuwa watu wote waruhusiwe kupata maji hayo pasi na kutoa pesa zozote (*no money*). Hii iliwafanya wenyeji kuanza kupaita *Itangini (kwa Nomani)*. Tangi hilo halitumiki tena lakini bado liko.

*Manooni* ni jina linalotaja kijiji kilicho katika kata ya Kivani. Linarejelea aina fulani ya mawe yaliyo na uwezo wa kutia vifaa vya chuma makali. Vifaa hivi ni kama; mishale, mikuki, visu, mapanga na mashoka. Kwa mujibu wa wenyeji, mawe haya yalipatikana kwa wingi katika eneo maalumu ambapo wazee wangesafiri kwenda ili kutia vifaa vyao makali. Kwa hivyo jina hilo linaafiki sifa ya mahali penyewe. Japo kumetokea vifaa vya kisasa vya kutia vifaa makali, mawe hayo yangali yanatumika. Wakamba walihitaji mikuki, mishale na panga katika vita vyao dhidi ya Wamaasai ambao walikuwa wakiwavamia mara kwa mara na kuwaibia mifugo. Nao pia wangewashambulia Wamaasai kulipiza kisasi. Kwa hivyo iliwabidi wawe na zana kali za kivita. Aidha, walihitaji panga na mashoka ili kufanya kazi katika mashamba yao.

Walitumia ala hizi ili kufyeka misitu walipotaka kupanua mashamba yao. Nyua za mashamba yao na boma zilitengenezwa kwa matawi ya miti yenye miiba ambayo ilihitaji mapanga yenye makali na mashoka ili kuyakata na kuyatenganisha.

**HITIMISHO**

Makala hii imeshughulikia vigezo vya utoaji wa majina ya mahali katika jamii ya Wakamba. Kutokana na uchunguzi huu, imebainika kwamba kulikuwa na vigezo maalumu vilivyoongoza utoaji wa toponemia katika jamii ya Wakamba. Makala hii imebainisha vigezo vitano ambavyo ni: *shughuli za kijamii, majina ya miti na mimea tofauti, sifa za kimaumbile, majina ya ndege na wanyama, majina ya watu maarufu na upatikanaji wa vitu maalum*. Utaratibu huu wa utoaji wa majina ya mahali ulidhihirisha kwamba jamii ya Wakamba haikupata majina yake kiholela bali kwa kuzingatia vigezo maalumu na venye maana.

**Marejeleo**


Buberwa, A. (2011). *Viambishi Ngeli Katika Nomino za Pekee: Mifano Katika Majina ya Pekee ya Kiaya,* Kiswahili Juz. 74. Kur. 41-48.

Crystal, D. (1987). *The Camridge Encyclopedia of Language*. Cambridge. Cambridge University Press.

Habwe, J., Karanja, P. (2007). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahi*. Nairobi. Phoenix Publishers.

Kahigi, K. (2007). Ujanibishaji wa Office 2003 na Windows XP kwa Kiswahili sanifu katka *Kioo cha Lugha. Jarida la Kiswahili na Fasihi. Juzuu la 5. Idara ya Kiswahili,* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Karama, M. (2021). "Ni Mvita ni Mvita? Uchanganuzi wa usuli wa Toponimu za Mitaa ya Mombasa, Kenya." *East African Journal of Swahili Studies. Vol. 3(1)* (pp. 78-90).

Kihore, P. na Wenzake, (2004). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu: Sekondari na Vyuo*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.TUKI.

Kirui, R. (2013). "A Morpho-semantic Study of Kipsigis Toponyms". MA Thesis. Kenyatta University. Unpublised.

Kothari, C. (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques.* New Delhi. New Age

Masamba, D. (2004). *Sarufi Misingi ya Kiswahili Sanifu*. Nairobi. Phoenix. Publishers.

Mathooko, P.M. (2004). "An Integrated Perspective of Language Accomodation; A case study of Kikamba and Kitharaka". PhD Thesis, Kenyatta University. Unpublished.

Michemi, D. et al, (2022). "Ubainishaji wa Vigezo vya Utoaji wa Toponemia Katika Jamii: Mfano Kutoka Jimbo dogo la Maara Nchini Kenya". *East African Journal of Education, Humanities and Literature* (Vol. 5/ Issue -9), Chuka University. (pp. 176-184).

Mjapelo, P. (2009). "Namna Ngeli Zinavyosaidia Kuunda mMajina ya Watu." Tasnifu ya Uzamili. C h u o Kikuu cha Dar es Salaam. Unpublished.

Musyimi, D. (2011). "Maana ya Majina ya Watu Katika Jamii ya Wakamba", Tasnifu ya shahada ya uzamili, Chuo kikuu cha Kenyatta. Nairobi. New Age International Publishers Ltd.

Mwanamseke, F. (2011). "Uainishaji wa Ngeli Katika Lugha ya Kibena." Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Haijachapishwa.

Raybum, A. (2010). *Place Names*. The Canadian Encyclopedia - Historical- Dominion.

Rugemalira, J. (2009). *A Grammar of Runyambo*, Dar es Saalam: Language of Tanzania Project. University of Dar es Salaam.

Rye, J. (2006). *A Popular Guide to Norfolk Place Names*. Guist Bottom. Larks Press.

Sperber, D. na Wilson, D. (1995). *The Handbook of Pragmatics.* London. Blackwell.

Wambua, R. (2013). *WONI WITU: The role of the Akamba in the making of Kenya*. Nairobi. Edtech Strategies Ltd.